TANZANIA REVENUE AUTHORITY

MABADILIKO KATIKA SHERIA ZA KODI YALIYOFANYIKA KWENYE SHERIA YA FEDHA YA MWAKA 2010

Katika hotuba ya Bajeti ya mwaka 2010/11 Serikali imefanya mabadiliko mbali mbali katika sheria za Kodi kwa nia ya kufanya maboresho kwenye usimamizi wa kodi zinazosimamiwa na TRA. Mabadiliko hayo ni pamoja na kuongeza na kupunguza baadhi ya misamaha ya kodi, kuongeza au kupunguza unafuu wa kodi ya ongezeko la thamani. Sheria zilizo na mabadiliko haya ya viwango vya kodi ni kama zifuatavyo:-

1. Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), Sura 148
2. Kodi ya Mapato, Sura 332
3. Ushuru wa Bidhaa, Sura 147
4. Sheria ya Magari (Kodi ya usajili na Uhamisho wa umiliki wa magari), Sura 124
5. Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004

A Mabadiliko katika Sheria ya Kodi ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT):

Katika sheria ya kodi ya ongezeko la thamani kumefanyika mabadiliko yafuatayo:-

Misamaha ya VAT

i. Usafirishaji wa mazao ya kilimo kutoka shambani hadi Kwenye viwanda vya usindikaji kwa wakulima wenye kilimo cha mkataba wa miwa, mkonge na chai;

ii. Mashine na vifaa vya kukusanya, kusafirisha na kusindika maziwa. Mashine na vifaa vitakavyohusika na msamaha ni:-
   (a) Vifaa maalum vya kubebea maziwa (Milk cans- HS Code: 7310.29.90)
   (b) Pampu maalum za kusukuma maziwa (Milk pumps- HS Code no. 8413.81.00);

   (c) Bomba maalum la kupitishia maziwa Kwenye viwanda vya usindikaji (Milk hoses- HS Code no. 8413.70.20);

   (d) Kompresser maalum zinazotumika Kwenye vifaa vya kupoza maziwa (Compressors used in refrigerating equipment-HS Code no. 8414.30.00)

   (e) Matanki ya kuhifadhia maziwa (Storage tanks- HS Code no. 7309.00.00);

   (f) Gari maalum lenye kifaa cha kupoza na kusafirisha maziwa (HS Code 8716.31.90);

(g) Mtambo maalum wa kuchemsha maziwa (milk pasteurizers- HS Code no. 8434.20.00);

(h) Kifaa maalum cha kuchekecha maziwa ili kutoa siagi (Butter churns- HS Code 8434.90.00);

(i) Vifaa maalum vya kupoza na kutengeneza ubaridi – HS Code no. 8415.81.00);

(j) Kifaa maalum cha kukandamiza mabonge ya maziwa na kukamua maji ili kuzalisha jibini (Chees pressers - HS Code no. 8434.20.00).

iii. Mashudu kwa ajili ya chakula cha mifugo,

iv. Zana za kilimo kama vile Kivuna nafaka (combine harvester), pick up balers, hay making machinery na mowers vinavyotumika mahsusi kwenye uzalishaji wa kilimo na mifugo

v. Usafirishaji wa maua kwa ndege kwenda nje ya nchi

vi. Huduma za kuzalisha mifugo (breeding services) kwa njia ya kupandisha mifugo na kutumia mashine maalum za kuzalishia/ kutotolea vifaranga (incubators);

vii. Kusamehe kodi kwenye vifungashio vya juisi za matunda na bidhaa za maziwa

Unafuu maalumu (VAT special Relief)

(i) Vifaa vinavyouzwa kwa wataalam wa mifugo waliosajiliwa. Unafuu huu utolewe katika Jedwali la tatu katika badala ya sasa Jedwali la pili (exempt Supplies)

(ii) Mabanda yanayotumika katika kilimo cha maua (green houses);

(iii) Uuzaji wa bidhaa na huduma kwa wakulima waliosajiliwa au mashamba ya vyama vya ushirika kwa ajili ya kujenga miundo mbinu ya mashamba kama vile mitaro ya umwagiliaji, barabara za mashambani, ujenzi wa maghala au huduma nyingine za namna hiyo;

(iv) Waendelezaji wa maeneo ya uwekezaji ya EPZ/SEZ

(v) Kurejesha utaratibu wa kutambua baadhi ya vifaa kama bidhaa za mitaji (Deemed Capital Goods) kwa baadhi ya wawekezaji. Serikali itaunda kamati maalum itakayosimamiwa na TRA ili kufuatilia na Kuratibu mchakato wa utoaji wa unafuu Pamoja na Udhibiti na matumizi yake.

VAT kwa kiwango cha Sifuri

Kutoza VAT kwa kiwango cha Sifuri Kwenye usindikaji na uzalishaji wa mafuta ya kula kwa wazalishaji wanaotumia mbegu za mafuta zinazozalishwa hapa Nchini.

B: Mabadiliko katika Sheria ya Kodi ya Mapato- Sura 332

(i) Kuweka wigo wa ukomo (ring fencing) wa maeneo ya uchimbaji wa Madini kwa nia ya kudhibiti gharama zinazotakiwa kutolewa katika kukokotoa faida itakayotozwa kodi ya Mapato kuwa zile za maeneo husika tu. Hatua hii itahusisha kampuni zote za Madini.

(ii) Kupunguza kiwango cha chini cha kodi ya Mapato kwa wafanyakazi kutoka asilimia 15 hadi asilimia 14;

VIWANGO VYA KODI KWA WATU BINAFSI WAKAZI KUANZIA TAREHE 1/7/2010

Na.	MAPATO YA KUTOZWA KODI KWA MWEZI	KIWANGO CHA KODI
1	Mapato yasiyozidi sh. 135,000/=	Hakuna Kodi
2	Mapato yanayozidi sh. 135,000/= lakini hayazidi sh. 360,000/=	14% ya kiasi kinachozidi sh. 135,000/=
3	Mapato yanayozidi sh. 360,000/= lakini hayazidi sh. 540,000/=	Sh. 31,500/= ongeza 20% ya kiasi kinachozidi sh. 360,000/=
4	Mapato yanayozidi sh. 540,000/= lakini hayazidi sh. 720,000/=	Sh. 67,500/= ongeza 25% ya kiasi kinachozidi sh. 540,000/=
5	Mapato yanayozidi sh. 720,000/=	Sh. 112,500/= ongeza 30% ya kiasi kinachozidi sh. 720 ,000/=

(iii) Kutoza kodi ya zuio kwa wauzaji wa bidhaa na watoa huduma wasiokuwa na TIN izuiwe pia na wafanyabiashara wote waliosajiliwa ili kuhamasisha wasiosajiliwa wajisajili.

C: Mabadiliko katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147

i. Kupunguza Ushuru wa bidhaa Kwenye mafuta mazito ya kuendesha mitambo kutoka shilingi 97 hadi shilingi 80 kwa lita;

ii. Marekebisho ya asilimia 8 ya viwango maalumu ya ushuru wa bidhaa – isipokuwa bidhaa za mapato ya Petroli.

VIWANGO VYA USHURU WA BIDHAA

SN	**Aina ya bidhaa**	**Kiwango cha zamani Tsh.**	**Kiwango kipya cha sh.**
1.0	Mafuta mazito ya kuendesha mitambo	97 kwa lita	80 Kwan lita
2.0	Vinywaji baridi visivyo na kilevi kwa kila lita	58 kwa lita	63 kwa lita
3.0	Bia inayotengenezwa na nafaka ya hapa nchini na haijaoteshwa	209 kwa lita	226 kwa lita
4.0	Bia nyingine zote	354 kwa lita	382 kwa lita
5.0	Mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango knachozidi asilimia 25%	1,132 kwa lita	1,223 kwa lita
6.0	Vinywaji vikali	1,678 kwa lita	1,812 kwa lita
Viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye Sigara		**Kwa sigara 1000**	**Kwa sigara 1000**
7.0	Sigara zisizo na kichungi na kutengenezwa na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha 75%	5,749	6,209
8.0	Sigaza zenye kichungi zinazotengenezwa na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa 75%	13,564	14,649
9.0	Sigara nyingine zenye sifa tofauti 7 & 8	24,633	26,604
10.0	Tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza Sigara (cut filler)	12,441	13,436
11.0	Ushuru wa Cigar unabaki kuwa asilimia 30		

D. Mabadiliko katika Sheria ya Magari (Kodi ya Usajili na Uhamisho wa Umiliki wa Magari)- Sura 124

Sn	Aina usajili	Ada ya sasa	Ada mpya
1	Kusajili magari	120,000/=	150,000/=
2	Kusajili pikipiki	35,000/=	45,000/=

E Mabadiliko katika Sheria ya Usalama barabarani, Sura 168

SN	Ujazo wa Injini	Kiwango cha zamani Tsh.	Kiwango kipya cha sh.
1	0 – 500. cc	30,000/=	50,000/=
2	501- 1500.cc	50,000/=	100,000/=
3	1501- 2500.cc	100,000/=	150,000/=
4	Zaidi ya 2500.cc	150,000/=	200,000/=

F. Ushuru wa Forodha chini ya Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004

Viwango vya ushuru wa forodha

(i) Kuongeza ushuru wa Forodha kwenye vipitishi joto au umeme wa aluminium iliyo wazi na nyaya (bare aluminium conductors and cables) za HS Code no. 7614.10.00 na 7614.90.00 kutoka asilimia 10 hadi 25. Lengo ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo katika Jumuiya.

(ii) Kuongeza ushuru wa forodha kwa nyaya za umeme (HS Code no. 7413.00.90 kutoka asilimia 10 hadi 25 ili kuwianisha na ushuru unaotozwa kwa shaba nyekundu (Copper wire) ambayo ni bidhaa shindani.

(iii) Kuondoa ushuru kwenye malighafi zinazotumiwa katika uzalishaji wa bidhaa zenye msamaha. Lengo ni kuweka mazingira mazuri ya kiushindani Baadhi zilikuwa zikitozwa ushuru wa asilimia 10 au 25.

(iv) Kupunguza kiwango cha ushuru wa pamoja kutoka asilimia 10 hadi 0 kwa malighafi ya viwanda vya kutengeneza rangi (driers) inayotambuliwa chini ya HS Code no. 3211.00.00;

(v) Kupunguza kiwango cha ushuru wa pamoja wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi 0 kwa malighafi za viwanda vya saruji (Petroleum coke, not calcined) HS Code no. 2713.11.00

(vi) Kupunguza kiwango cha ushuru wa pamoja wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi 0 kwenye malighafi zinazotengeneza kadi zinazotumiwa na makampuni ya simu kuuza muda wa maongezi (Stamping foils) HS Code no. 3212.10.00;

(vii) Kupunguza kiwango cha ushuru wa pamoja wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi 0 kwenye malighafi ya viwanda vya kutengeneza rangi inayotambuliwa chini ya HS Code no. 3212.90.10

(viii) Kupunguza kiwango cha ushuru wa pamoja wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi 0 kwenye malighafi ya viwanda vya vyuma. HS Code no. 7210.11.00; na HS Code no. 7212.10.00;

(ix) Kupunguza kiwango cha ushuru wa pamoja wa Forodha kwa majiko yanayotumia gesi kutoka asilimia 25 hadi 10 (HS Code no. 7321.11.00);

(x) Kutoza ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya 35 kwenye ngano inayotambulika chini ya HS Code no. 1001.90.20 na HS Code no. 1001.90.90 kwa muda wa mwaka mmoja kwa vile nchi Jumuiya bado hazijaweza kukidhi mahitaji ya soko la ndani.

(xi) Kutoza ushuru wa Forodha wa asilimia 10 badala ya 25 kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa magari yenye uwezo wa kubeba tani 5 lakini hayazidi tani ishirini kama vile Fuso, isuzu nk. Inayotambulika chin ya HS Code no 8704.22.00;

(xii) Kutoza ushuru wa Forodha wa asilimia 0 badala ya 25 kwa magari yenye uwezo wa kubeba zaidi ya tani 20 HS Code no. 8704.23.90;

(xiii) Kutoza ushuru wa Forodha wa asilimia 25, HS Code no. 2523.29.00
kwenye saruji kwa muda wa mwaka mmoja;

(xiv) Kutoza kiwango cha ushuru wa pamoja wa forodha cha asilimia 35 au Dola za Kimarekani 0.20 (U$ 0.20) kwa kilo kwa nguo za mitumba (HS Code no. 6309.00.00)

(xv) Kupunguza Ushuru wa forodha kwa mabasi yatakayoingizwa Nchini kwenye mradi wa mabasi yaendayo kasi (Fast Truck Bus Project) HS Code 8702.10.99 na 8702.90.99 na kwa 10%

(xvi) Ushuru wa forodha kwa matrekta ya kukokota matrekta yanayotambulika chini ya HS Code no. 870.20.90 ushuru umepunguzwa kutoka 10% hadi 0%

Msamaha wa ushuru wa forodha

(i) Ushuru wa forodha kwa kutumia utaratibu wa “Duty Remission Scheme” malighafi za kutengeneza majalada na vitabu (Textile garments coated with gum) HS Code no. 5901.10.00.

(ii) Ushuru wa Forodha kwa kutumia utaratibu wa “ Duty Remission Scheme” malighafi za kutengeneza viatu (Looped pile fabrics of manmade fibres) HS Code no. 6001.22.00;

(iii) Ushuru wa forodha kwa waunganishaji wa magari (Motor Vehicles Assemblers)

(iv) Ushuru kwenye kuku wazazi (parent stock) HS Code no.0105.99.00 Lengo kuhamasisha sekta ya ufugaji wa kuku;

(v) Ushuru wa forodha kwenye taa/balbu zinazotengenezwa kwa kutumia technologia ya Emitting Diodes (LED) lengo ni kuhamasisha matumizi madogo ya umeme;

(vi) Kutotoza ushuru kwa bidhaa zinazouzwa kwenye migahawa ya Majeshi ya Ulinzi na usalama (Armed Forces Canteen) kwa mwaka mmoja;

(vii) Ushuru wa forodha kwa glavu (examination gloves) zinazotumika katika hospitali na maabara HS Code no. 4015.19.00;

Marekebisho kwenye msamaha jedwali la 5 la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kwa wananchi wanaorejea Nchini (returning residents) kipindi cha miaka minne (4), kabla mwombaji hajapata msamaha mwingine wa namna hiyo.

G. Ushuru wa Korosho Sura ya 203

Ushuru wa kusafirisha nje (Export levy) korosho ghafi umeongezwa kutoka asilimia 10 hadi asilimia 15 ya thamani kabla ya kusafirishwa nje (FOB) au dola za Kimarekani 160 ($160) kwa tani moja kutegemea kiwango kipi ni kikubwa. 65% ya makusanyo ya ushuru huu yatagawanywa kwa halimashauri za wilaya husika

Imetayarishwa na
Idara ya Huduma na Elimu kwa mlipakodi
25 Juni 2010